JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZAN

OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI


NAMBA ZA SIMU
Mkuu wa shule 0765715326/0756304736
Makamu 0787 13 95 28 / 0624 03 56 73
Matron/Patron 0622000331


Mzazi /Mlezi wa Mwanafunzi ..........................................................................

S.L.P ........................................................................................................

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI PROF. JOYCE NDALICHAKO HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA MKOA WA KAGERA MWAKA …….

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……….. na atasoma tahasusi ya ……….…

Shule ya Sekondari **PROF. JOYCE NDALICHAKO** ipo umbali wa Kilometa 14 kutoka Muleba mjini (barabara iendayo Biharamulo,mwanza ama kahama). Shule ipo katika kata ya RULANDA (shukia kituo cha mabasi Rulanda, pia unaweza kushukia kwenye kibao cha shule PROF. JOYCE NDALICHAKO ili kuepusha usumbufu). Nauli toka Muleba mjini ni tsh 2000/=

Muhula wa masomo unaanza tarehe ……….. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 05/07/2026 mwisho wa kuripoti ni tarehe ………….

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

2.1 **Sare za Shule**

(i) Shati nyeupe 2 aina ya tomato zenye mikono mirefu na zisizo na urembo wowote.

(ii) Soksi nyeupe jozi 2 (stocking).

(iii) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi, vyenye kufunika miguu na visivyo na urembo wowote, jozi 2. (Siyo mfano wa buti )

(iv) Nguo za michezo ambazo ni “track suit” ya kijivu kitambaa kizito kisichoteleza, isiyobana na isiyo na kofia na raba nyeupe (Siyo mfano wa buti), jozi moja.

(v) Sweta rangi nyekundu. shingo ya “V” ikiwa na nembo ya shule upande wa kushoto (inapatikana shuleni).

(vi) Tai mbili zenye kufanana na rangi za sketi.

(vii) Sketi mbili

I, Kitambaa cha draft nyekundu na nyeupe (2). Dark blue kitambaa kizito (Esteem). ( ziwe na mshono wa “malinda” jumla ya malinda yawe kumi, mbele matano na nyuma Matano. Sketi ivuke magoti kwa inch saba).( Picha imeambatanishwa)

(viii) Nguo za nje ya darasa (shamba dress). Gauni (2), 1. rangi ya kijivu (Grey) na 2. Zambalau ( kitambaa cha tetron nzito au Esteem na siyo aina nyingine ya kitambaa. Mshono wa soro na shingo ya duara, Gauni ivuke magoti inch saba).

(ix) “T- Shirt” mbili (2), 1. rangi ya pink yenye kola yenye kitambaa Kizito (form six) yenye nembo ya shule mbele na nyuma. (Inapatikana shuleni). Tshrt 1 Rangi ya blue shingo round isiyo na mandishi yoyote kwa ajili ya michezo .

(x) Rangi ya hijab (kijuba) nyeupe na pink ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (Picha imeambatanishwa).

(xi) Wenye changamoto ya kifua aje na cheti lakini pia aje na PULL NECK (nyeupe)

TANIBIHI Mwanafunz aje amevaa mojawapo ya sare za shule tajwa hapo juu asije na nguo yoyote ya nyumbani.

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

(i) Madaftari makubwa yasiyopungua 10 (counter books)
(ii) Mkebe wa Hisabati (Mathematical set)
(iii) Rula, kalamu za wino na pencil za kutosha muhula
(iv) Dictionary/Kamusi (kwa wanafunzi wa sanaa)
(v) Karatasi (Photocopy papers-double A) Ream 2 kwa mwaka.
(vi) Scientific Calculator (wanafunzi wa sayansi)- zipo maduka karibu na shule
(vii) Dissecting kit 1 na Dissecting tray 1 kwa wanafunzi wa Biolojia
(viii) Mwavuli wa mvua mmoja (1).
(ix) Mto mmoja (1) na foronya mbili (2) za rangi ya pinki na blue
(x) Mashuka mawili (2 ). Moja la pinki na jingine la blue yasiyo na maua na blanketi moja (1).
(xi) Godoro moja (1) la futi 2½ na chandarua moja (1) nyeupe (ya duara)
(xii) Nguo ya kulalia (night dress)
(xiii) Jozi moja (1) ya vitenge.
(xiv) Sahani 1, bakuli 1, kikombe 1, kijiko 1,
(xiv) Toilet papers (karatasi za chooni) kumi (10).
(xv) Kifaa cha kutunzia maji ya kunywa.
(xvi) Taulo moja (1).
(xvii) Tochi moja (ya kuchaji kwa jua)
(xviii) Nguo za ndani (gagulo (underskirt) chupi za kutosha na sidiria 3.(nyeusi au

nyeupe).

(xix) Taulo za kike zisizopungua paketi 6.

(xx) Sabuni, mswaki, dawa ya meno,mafuta ya kujipaka, dawa ya viatu.

(xxi) Jembe 1 lenye mpini, mifagio 2 wa ndani na nje, brashi kwa ajili ya usafi wa vyoo na bafu (Squeezer/Fraps 1 & hard brush 1)

(xxii) Ndoo ya kuchotea maji yenye ujazo wa lita 20 na ndoo ndogo ya lita 10 moja ya kuogea

(xxiii) Box file kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake za mitihani (mali ya mwanafunzi)

(xxiv) Mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya (ambaye hana bima aje na tsh 50,400 ili shule ifanye utaratibu wa kukata bima za wanafunzi) HILI NI MUHIMU NA LITAKAGULIWA

MWANAFUNZI AJE NA MOJA YA VITABU VIFUATAVYO VYA KILA SOMO KULINAGANA NA TAHASUSI YAKE.

**PHYSICS REFERENCE BOOKS**

1. Mastering physcis phase one and phase two advanced level
2. Metha V.k, (2013) S.Chand's principles of PHYSCICS for class XII 7th ED, S.Chand & Company Pvt.Ltd, New Delh

3 TIE books new syllabus form five

**CHEMISTRY REFERENCE BOOKS**

1. Jain S.K, (2010), Conceptual chemistry for class xl s. Chand & company Ltd, New Delhi, India
2. Mkayula, L.L et al ( 1998), physical, chemistry. Volume 1, ( mzumbe Book Project) Mzumbe, Tanzania.

3 TIE books form five new syllabus

4. Bahl B.S et al (2009) Essential of physical chemistry S. Chad & company Ltd, New Delhi, India.
5. Ramsden. E.N(2000), A – level chemistry, 4th Ed, Nelson Thornes Ltd U.K

**BIOLOGY REFERENCE BOOK.**

2) D.J,(1999), Biology Science, 3rd Ed,Cambridge Unverstity PressLondon

1. TIE books new syllabus.

**GEOGRAPHY BOOKS**

1. Mcknight T, (2008) Physical Geography A L and scape appereciation prentice Hall USA.
2. Pritichard J, (1984), Physical Geography for Africa, Longman group U.K
3. Bunnet R,( 1973), General Geography in Diagram, Education Singapore.
4. Monkhouse, F(1975) Principal of physical Geography, Education Hodder, UK

5 TIE books new syllabus form five

**GENERAL STUDIES**

1. Understanding general studies 3rd Edition for advanced level ( JOANES BIGIRWAMUNGU

2 TIE form five new syllabus

## HISTORY BOOKS

1) TIE advance level new syllabus
2) Yassin salehe essential in advanced level history paper 1 Dar es salaam
3) Contemporary historical events advanced level history 2 by comred shibital c.k Tumain( Third edition)
4) Yassin salehe essential in advanced level history paper 2 Dar es salaam

## ENGLISH LANGUAGE 1

1) TIE new syllabus form five
2) Asheri 2014 advanced level English
3) Advanced English oxford longman dictionary

**ENGLISH LANGUAGE 11**

1) TIE new syllabus form five
2) Ashel N 2014 advanced literature

**ANGALIZO- Maandalizi ya mtoto wako yalenge mtaala ulioboreshwa na sio mtaala wa zamani**

2.3 Michango

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

N B. Fedha hizo zote zilipwe kwenye akaunti ya shule:

PROF. JOYCE NDALICHAKO SECONDARY SCHOOL Namba ya akaunt 32010010083 Benki ya NMB. Mwanafunzi awasilishe nakala ya RISITI ya malipo iliyoandikwa jina lake wakati wa kuripoti.

3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu — TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

-  Mwanafunz hapaswi ku a na simu shu eni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunz

-  Mwanafunz awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni al lopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunz ku ala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunz mmoja tu

-  Mwanafunz ataruhusiwa kurud nyumbani kwa ruhusa na kibal maalum toka kwa Mkuu wa Shu e. (Msiba wa baba/mama, dada/kaka wa tumbo moja au ugonjwa).

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunz kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;(shu e yetu inaruhusu kusuka kwa wanafunz wa kidato cha tano na sita tu aidha mt ndo wa kusuka ni nywele za misitari(twende kilioni) isiyoz d mitano au saba bila nyuz ).

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kupewa taarifa za mwanafunzi pamoja na Namba zao za Simu.
v. Mwanafunzi alete nakala ya hati ya matokeo (result slip) yake ya kidato cha nne akiwa ametoa ‘copy’

NB: Utumaji wa fedha binafsi za mwanafunzi yako
Wazazi wanaowatumia watoto wao fedha za matumizi wafanye hivyo kwa kutumia njia ya

Mkuu wa shule 0753959981/0621619193 (MBABAZI BUNINANGE) ,taarifa za kuwataka

wanafunzi kufuata fedha zilizotumwa kupitia kwa jamaa zao wanaokaa nje ya shule

hazitakubaliwa

NB; Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wiz kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazaz wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzaz husika ambaye pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZ /MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI NA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO;

- Mkuu wa shule– **ANTIDIUS R. KAMAZIMA(0765715326/0756304736)**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0624035673**
- **Matron 0622000331**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**…………………….**
**ANTIDIUS R.KAMAZIMA**
**MKU WA SHULE**

.

## TAARIFA BINAFSI

A. Jina la Mwanafunzi ..........................................................................................

Anwani ya nyumbani ..........................................................................................

........................................................................................................................ Kabila .......................................... Tarehe ya kuzaliwa ........./.........../20............

Mtanzania /Si Mtanzania

Dini ya Mwanafunzi................... Mtaa/Kijiji .........................................Jina la mratibu elimu kata/mtendaji za………………….simu..……......Wilaya.....................Mkoa.............

B. Jina la Baba .................................................. * (Hai/Marehemu) .......................

(Mwaka aliofariki) ............................. ……….

Dini ya Baba ............................ Kazi ya Baba ........................... Simu Na ..................

Jina la Mama ................................................. *(Hai/Marehemu) .............................

(Mwaka aliofariki)...................................

Dini ya Mama ............................. ....... Kazi ............................. Simu Na. .............

C. Taja majina na anuani za Walezi/Ndugu wengine wawili wasiokuwa wazazi wanaoruhusiwa kufika shuleni kusikiliza matatizo ya mtoto na kutoa maamuzi juu ya mashauri ya mtoto wako.

JINA................................................ Uhusiano .......................umri……..SIMU NA................................

JINA ............................................... Uhusiano........................umri………SIMU NA …………………….

MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE TECHNOLOGY AND VOCATIONAL

TRAINING FORM FOR STUDENT MEDICAL

EXAMINATION

Student's Name …………………………………………………………………………

Blood Examination: Haemoglobin …………………………Blood Group ………..

Stool Examination ……………………………………...………………………………

Urinalysis …………………………………………………..........………………….

Pregnancy test………………………………………………………………………...

T.B. Test (If negative, was immunization given)……………………………………..

Eyes……………………………………………………………………………

………….. Chest ……. Any chronic complaints not noted above e.g.

Asthma Headache

………………………………………..…………………..…………………

Inability to eat certain foods ………………….….. Skin diseases etc.................... Also anything that

the School health staff should know about………………………….

…………………………………………………………………………………………….

Any treatment given or recommended ……………………………………………..

………………………………………………………………………………………......

NOTES: If any of the examinations requested above cannot be carried out, it is useful if it is noted that they have not been done rather than writing NAD down. In case of Bilharzia it is recommended that students attend the Bilharzia clinic before they come to school.

Signature of Examiner

………………………… Designation

……………………………………..

Designation ……………………………………..

Date……………………………………………

